
Steps
Clubfoot Care

# Mguu kifundo unatibika!



**Muongozo wa hatua kwa hatua kwa wagonjwa wapya wa mguu kifundo**

**Tutatembea na wewe**




## MGUU KIFUNDO

- Hakuna kisababishi maalum kinachofahamika kinachoweza sababisha mtoto kuzaliwa na mguu kifundo. Aidha si kosa la mtu yeyote katika familia.
- Mguu kifundo ni moja ya ulemavu wa kuzaliwa.
- Mguu unakuwa na hali ya tofauti ukilinganisha na miguu ya watoto wengine kwa kuwa mgumu sana na muonekano wa tofauti kabisa.
- Mguu unakuwa umegeuka kiasi kwamba sehemu ya juu ya mguu inakuwa inaangalia chini na sehemu ya chini ya mguu inaangalia juu.
- Aidha mguu unakuwa umejikunja kuelekea chini na ndio maana kwa jina la kitaalamu ukaitwa MGUU KIFUNDO AU MGUU RUNGU kulingana na muonekano wake kufanania kufundo au rungu.
- Mguu kifundo unaathiri zaidi ya watoto 2 kati ya vizazi 1000 kila mara.
- Mguu kifundo unaweza kujitokeza kwa zaidi ya mtoto mmoja ndani ya familia lakini mpaka sasa hakuna uthibitisho wa kisayansi unao onyesha  kama ni ugonjwa wa kurithi.
- Aidha mguu kifundo unawaathiri zaidi watoto wa kiume kuliko watoto wa kike kwa uwiano wa 2 kwa 1.
- Mtoto alie na mguu kifundo ataangaliwa kama ana changamoto nyingine japokuwa kwa watoto wengi changamoto hii hujitokeza yenyewe.

### MATIBABU YA MGUU KIFUNDO YALIYOTHIBITISHWA ULIMWENGUNI NI KUTUMIA MUONGOZO WA PONSETI

## MATIBABU YA MGUU KIFUNDO KWA MUONGOZO WA PONSETI

Zaidi ya asimilia 95 ya matibabu kwa njia ya Ponseti yamefanikiwa. Kama muongozo wa matibabu ya PONSETI utafuatwa vyema,  basi ni dhahiri mtoto atapona kabisa.

1. Chezesha viungo vya mguu taratibu uweze kulainika
2. Muhogo utabadilishwa kila wiki ndani ya wiki 4 mpaka 6
3. Asilimia 80 ya watoto wenye mguu kifundo wanahitaji upasuaji mdogo wa mshipa wa kisigino
4. Baada ya upasuaji mdogo wa mshipa wa kisigino, mtoto atafungwa muhogo awamu ya mwisho.
5. Mtoto ataanza kutumia viatu tiba baada tu ya muhogo wa awamu ya mwisho kutolewa.
6. Viatu tiba vitavaliwa ndani ya masaa 23 kwa siku, kwa muda wa miezi 3 mwanzo.
7. Baada ya miezi 3 kukamilika, viatu tiba vitavaliwa usiku na muda wa mtoto kulala tu kwa siku ( masaa 12 hadi  14 kwa siku)
8. mtoto atapaswa kuvaa viatu tiba  mpaka atakapofikisha umri miaka 4


## KULAINISHA VIUNGO VYA MGUU NA KUFUNGA MUHOGO/PLASTA







- Muhogo hautamuumiza mtoto wako.
- Muhogo utafungwa kuanzia kwenye vidole mpaka kwenye nyonga, sehemu goti ikiwa imekunjwa.
- Mlete mtoto akiwa na njaa ili wakati wa kufungwa muhogo awe ananyonya, kutampa faraja.
- Muhogo mbichi ni mzito. Kunja taulo kisha uweke nyuma ya magoti yake kumpa egemeo mpaka muhogo ukauke.
- Muhogo utabadilishwa kila baada ya wiki moja , utatolewa katika eneo la kliniki masaa machache kabla ya kufunga mwingine.
- Muhogo utafungwa kila wiki mpaka mguu wa mtoto uwe katika hali ya kawaida.

## UPASUAJI MDOGO WA  MSHIPA WA KISIGINO



- Watoto wengi wa mguu kifundo wana mshipa mfupi wa kisigino
- Bila upasuaji mdogo wa mshipa wa kisigino mtoto atatembelea vidole vya mguu
- Huu ni upasuaji mdogo kwenye mshipa wa kisigino cha mtoto mwenye mguu kifundo. Mshipa huu huwa mfupi hivyo upasuaji  mdogo unalenga kuongeza urefu wake ili kumalizia marekebisho ya mwisho ya Mguu kifundo
- Unafanyika kwa kutumia ganzi ndogo katika eneo la upasuaji, inachukua dakika 10 tu
- Baada ya upasuaji mdogo , muhogo wa awamu ya mwisho utafungwa na utakaa kwa muda wa wiki 3
- Baadhi ya madaktari hutumia ganzi ya mwili mzima kwa watoto wakubwa
- Unaweza mpa mtoto dawa ya maumivu baada ya upasuaji huu


## UTUNZAJI WA MUHOGO/PLASTA NYUMBANI



- Hakikisha plasta ni safi na kavu muda wote
- Usimuogeshe mtoto
- Tumia kitambaa chenye sabuni na maji kumsafisha mtoto



- Kagua kama muhogo au plasta kama ina ufa au imekatika sehemu yeyote
- Usiweke kitu chochote ndani ya muhogo.



- Unapaswa kuona vidole vya miguu muda wote
- Vidole vinapaswa kuwa na joto la mwili la kawaida na rangi halisi ya ngozi
- Bonyeza vidole kila baada ya masaa kadhaa kuhakikisha mzunguko wa damu upo vizuri






- Unaweza mvalisha mtoto soksi juu ya muhogo kama hali ya hewa ni ya ubaridi
- Weka egemeo (taulo) chini ya magoti ya mtoto kumuwezesha kulala vizuri

## CHANGAMOTO ZA MUHOGO/PLASTA

Wasiliana na daktari wako au rudi kliniki ikiwa utaona dalili yoyote kati ya yafuatayo;





- Homa kali
- Uvimbe juu au chini muhogo ulipofungwa
- Vidole vya miguu kuvimba.
- Muhogo/plasta kubana sana mguu
- Harufu mbaya toka ndani ya plasta/muhogo
- Vidole kupooza au kupoteza joto la mwili
- Vidole vya miguu kupoteza rangi yake ya kawaida
- Mguu kuteleza na kutoka nje ya muhogo/plasta baada ya kufungwa
- Vidole kutoonekana baada ya kufungwa muhogo/plasta
- Muhogo kuharibika na kupoteza ubora wake kabla ya tarehe ya miadi ya kliniki
- Muhogo/plasta kutoka na kuuacha mguu bila marekebisho

## KUONDOA MUHOGO






- Kliniki zingine zina utaratibu wa kuondoa muhogo wenyewe, na zingine zitakufundisha namna ya kuondoa muhogo kwa mtoto
- Usitoe muhogo usiku wa kuamkia siku ya kliniki
- Paka maji muhogo kasha funika na kitambaa chenye unyevunyevu, na funika na mfuko wa plastiki ili kuilainisha plasta/muhogo
- Unapaswa kupata kifundo cha plasta/muhogo karibu na goti ili kukusaidia kuifungua kwa haraka na wepesi
- Ongeza siki kwenye maji italainisha plasta/muhogo haraka
- Kama ukifungua plasta/muhogo katika kliniki utapata huduma ya chombo cha kufungulia pamoja na maji ya moto

**Ukiwa kama mlezi au mzazi wa mtoto, unajukumu muhimu katika mafanikio ya tiba ya mtoto (mguu kifundo). Ukiwa una maswali au wasiwasi, tafadhali wasiliana na mshauri wako wa kliniki au wa wazazi.**


### TAARIFA ZA KLINIKI

### UFUNGAJI WA MUHOGO




| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

### UFUNGAJI WA MUHOGO




| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

### KIATU TIBA



| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

### KIATU TIBA



| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |